

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 022 2126826
Nukushi: 022 2126834
Tovuti: www.habari.go.tz
Baruapepe: km@habari.go.tz



Jengo la LAPF
Ghorofa ya Nane,
S. L. P. 25,
Makole Uhindini,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) amepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mwanasanaa na mchongaji Bw. Focus Senya Nampumu kilichotokea jana Juni 05, 2018 Jijini Dar es Salaam.

“Nimesikitisha na taarifa za kifo cha Mwanasanaa na mchongaji nguli ukizingatia alikuwa mstari wa mbele kuhakikisha sanaa hii inajulikana kwa kuanzisha chama cha wachongaji cha vinyago (CHAWASAWATA)” alisema Dkt. Mwakyembe.

Enzi za uhai wake Bw. Focus Nampumu alishiriki katika shughuli mbalimbali za kuhamasisha uchongaji wa vinyago ikiwemo kuanzisha chama cha wachonga vinyango, pia alikuwa mwanaharakati wa kuwatetea wachongaji katika kuhakikisha wanapata ustawi wa biashara ya sanaa hiyo, ualimu pamoja na masoko.

Pia, marehemu aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya ushauri wa uundaji wa Shirikisho la Sanaa na Ufundi nchini, kushiriki katika tafiti zinazohusu uchongaji, sanaa, mazingira na biashara ya vinyago, pamoja na kushiriki katika kuanzisha mradi wa shule ya uchongaji Bagamoyo (*Bagamoyo Sculpture School*).

Dkt. Mwakyembe ametoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na uongozi wa Chama Cha Wachongaji Tanzania na Shirikisho la Sanaa za Ufundi (TAFCA) kwa kumpoteza nguli wa Sanaa za Uchongaji.

Imetolewa na

Lorietha Laurence
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.
06/06/2018